# Muhtasari wa Literacy Pittsburgh

| Swali | Jibu swali ikiwa unasubiri darasa. | Jibu swali kama unasubiri mwalimu wa kujitolea. |
|---|---|---|
| **Nitasoma siku gani na saa ngapi?** | Darasa ni Jumatatu (siku ya kwanza)-Alhamisi(Siku ya Inne) asubuhi, Mchana na jioni. Shule ni mara mbili kwa wiki kwa saa 2 kila wakati, ama Jumatatu (siku ya kwanza) na Jumatano (siku ya tatu) AU Juma nne(siku ya pili) na Alhamisi (siku ya inne). Tuna darasa ya kibinafsi na ya kompyuta. | Wewe na mwalimu wako wa kujitolea mtaamua wapi na lini mtakutana. Lazima kukutana mara mbili kwa wiki kwa saa 2 kila wakati. Ni lazima mkutane mahali pa umma au kwenye kompyuta. Huwezi kukutana na mwalimu nyumbani kwako ama kwa mwalimu. |
| **Nitaanza darasa lini?** | Darasa huanza mwezi wa kwanza, mwezi wa pili, mwezi wa saba na mwezi wa kumi. Tutafanya tuwezavyo kukuingiza darasani katika robo ijayo. Itategemea kiwango chako na upatikanaji. | Tutaanza kukutafutia mwalimu sasa, lakini kuna orodha ya wanaosubiri. Wanafunzi wengi hulinganishwa na mkufunzi baada ya kusubiri kwa miezi 2-3, lakini inaweza kuwa ndefu au fupi. |
| **Sera ya mahudhurio ni ipi?** | Kuna orodha ndefu ya kusubiri. Ili kujiunga na darasa, lazima uwe tayari kujitolea kwa saa 4 kila wiki. Unatakiwa kuhudhuria 75% ya madarasa yao. Ukikosa zaidi ya hayo, utapoteza nafasi yako darasani. | Kuna orodha ndefu ya kusubiri. Lazima uwe tayari kujitolea kwa saa 4 kila wiki. Usipopiga simu, usijitokeze kwa mwalimu wako mara mbili kwa mwezi mmoja, tutamwachilia mkufunzi wako kwa mwanafunzi mwingine kwenye orodha ya wanaosubiri. |
| **Je, ikiwa siwezi kuja darasani?** | Unatarajiwa kuhudhuria kila darasa au kumwambia mwalimu wako kwa nini huwezi kuhudhuria. Ikiwa huwezi kwenda kwenye darasa lako, tafadhali mjulishe mwalimu wako **KABLA** ya darasa kuanza. Mwalimu wako atakuambia jinsi ya kuwasiliana nao. | Unatarajiwa kuhudhuria kila somo au kumwambia mwalimu wako kwa nini huwezi kuhudhuria. Iwapo huwezi kuhudhuria darasa lako, tafadhali mjulishe mwalimu wako angalau saa 2 **KABLA** ya darasa kuanza. Mwalimu wako atakuambia jinsi ya kuwasiliana nao. |

| Swali | Jibu la swali kwa wanafunzi wote |
|---|---|
| **Je! nitajuaje darasa langu litakapoanza?** | Tutakutumia ujumbe mfupi wa maandishi na barua pepe wakati darasa linapatikana. Barua pepe zote zitasema "Literacy Pittsburgh" katika mstari wa somo. Ujumbe wote wa SMS utaanza na "This is Literacy Pittsburgh." Tafadhali tafuta jumbe hizi na uzisome kwa makini! |
| **Je, unatoa huduma ya watoto?** | Hapana. Literacy Pittsburgh haitoi huduma ya watoto kwa mikutano au madarasa yoyote ya ana kwa ana. Utahitaji kupata mtu wa kuangalia watoto wako. Pia tunatoa darasa ya mtandaoni ili uweze kukaa nyumbani na watoto wako ikiwa ni lazima. |
| **Je nikihitaji usaidizi?** | Literacy Pittsburgh inaweza kuwasaidia wanafunzi wetu! Tuna washauri wa taaluma ambao wanaweza kukusaidia kupata kazi, na tuna waratibu wa huduma za wanafunzi ambao wanaweza kukusaidia na matatizo mengine, kama vile kuhitaji chakula, nyumba au malezi ya watoto. Unaweza kuomba usaidizi kwenye tovuti yetu ya wanafunzi chini ya "jobs" na "student support". www.LPstudent.com |
| **Je, niwasiliane na nani ikiwa nina maswali?** | Jina la mratibu wako ni ______________________<br>Nambari yao ya simu ni ______________________<br>Barua pepe yao ni ______________________ |